# TASAFIC

*Elimu na Umoja Tuijenge Tanzania*

2025

Tanzania Students Associations Federation in China| c/o. Tanzania Embassy in Beijing 8 LiangMa He Nan Lu, Sanlitun, 100600 Beijing, P.R. CHINA| TASAFICtc@gmail.com

*Kwa habari zaidi www.TASAFIC.com*


## TANZANIA YAIBUKA MSHINDI WA PILI MASHINDANO YA BEIJING WORLD CUP

Beijing world cup ni mashindano yanayo husisha mpira wa miguu pamoja na netball, ila kwa nyakati tofauti yamekuwa yakihusisha mpira wa miguu zaidi, mashindano haya hufanyika kila mwaka yakiwa na dhumuni la kuwaleta watu wenye desturi na mila tofauti pamoja hapa Beijing ili kuleta umoja na ushirikiano kwa watu wote. Kwa kipindi cha mwezi Mei 2025 mashindano haya yalihusisha mataifa tofauti huku timu ya mpira wa miguu ya Tanzania ikiwa kundi moja na mataifa kama Angola, Malaysia, pamoja na Mali.

Katika hatua ya makundi timu ya mpira wa miguu kutoka Tanzania ilifaniikiwa kuongoza kundi ikishinda mechi zote tatu na kufanikiwa kuingia hatua ya kumi na sita bora iliofanya wachezaji wajitume hadi hatua ya fainali. Katika fainali za kombe la Beijing world cup timu ya Tanzania ilikutana na timu ya taifa la Cape verde, hata hivyo Cape verde ilifanikiwa kutwaa ubingwa huo baada ya sare ya magoli iliopelekea uongezwaji wa muda na kisha hatua ya mikwaju ya penalti cape verde wakipata penalti saba huku Tanzania ikipata penalti sita na kuwezesha timu ya Tanzania kuwa washindi wa pili kati ya timu ishirini zilizo shiriki.





Watanzania waliojitokeza kwenye mashindano ya Beijing world cup kuishangalia timu ya Tanzania Beijing

## MAONI YA KOCHA WA TIMU YA TANZANIA BEIJING



**David Joseph**

Mashindano ya Beijing world cup ni mashindano mazuri na yenye mvuto, sisi kama watanzania tulitumia muda wetu kutangaza na kuinadi nchi yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuonesha umoja na ushirikiano wetu ikiwa ndio desturi na utamaduni wa mtanzania kushirikiana hata nnje ya mipaka ya nchi yetu pendwa, hata hivyo mashindano haya yalikuwa njia nzuri ya kutuleta pamoja watanzania waishio Beijing ili kufahamiana na kuongeza ari ya ushirikiano baina yetu.
Mimi kama kocha mkuu wa timu ya Tanzania nawapongeza waandaji wa mashindano haya pasipo kusahau nguvu kubwa iliooneshwa na watanzania waishio Beijing, ushirikiano huu tuendeleze hata nnje ya michezo. Naamini mwisho wa mashindano haya ya 2025 ndio mwanzo wa maandalizi ya kuelekea msimu ujao wa mashindano 2026 tuna ahidi mafanikio mazuri na makubwa kwa pande zote uwanjani na jamii kwa kuitangaza Tanzania yetu.










Wachezaji pamoja na bechi la ufundi baada ya kupokea medali za mshindi wa pili.

## WATANZANIA WAWAKILISHA VEMA KATIKA TAMASHA LA UTAMADAUNI CHUO CHA ZHEJIANG NORMAL UNIVERSITY

Tarehe 25 Aprili, 2025, Uwanja wa Maonesho wa Chuo cha Zhejiang normal university uligeuka kuwa jukwaa la utamaduni, likiwakutanisha wanafunzi kutoka mabara tofauti, Tanzania ikiwa miongoni mwa mataifa yaliyoshiriki, pamoja na nchi kama Msumbiji, Uganda, Zimbabwe, Pakistan, Kenya, Ghana, Cameroon, Nepal, Ufaransa, Japani, Djibouti, Nigeria, Vietnam, Urusi, na mataifa ya Asia ya Kati.

Tamasha hilo lilitoa fursa kwa wanafunzi kuonesha urithi wao kupitia utamaduni wa nchi zao ikijumuisha vyakula vya asili, mavazi ya kipekee, ngoma, muziki, na sanaa. Banda la Tanzania lilivutia wageni wengi, lilipambwa kwa rangi za bendera ya taifa na vitu vya kiutamaduni vilivyobeba hadhi ya taifa. Wageni walipata fursa ya kuonja vyakula vya asili kutoka Tanzania na kujifunza historia ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia maelezo ya wanafunzi.



Watanzania kutoka Zhejiang normal university wakiwa katika picha ya pamoja

Tamasha hili la Utamaduni katika Chuo Kikuu cha Zhejiang Normal University hufanyika kila mwaka katikati ya mwezi Aprili, likiwa na lengo la kutoa fursa kwa wanafunzi wa kimataifa kutoka mataifa mbalimbali kuonesha utamaduni wao.




Baadhi ya wanafunzi kutoka Tanzania katika picha ya pamoja na wanafunzi wa Uganda






Banda la maonesho likiwa na vyakula tofauti asili ya Tanzania



Moja ya wanafunzi wa Zhejiang normal University akionesha kwa furaha bendera ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nchi yetu fahari yetu.




Ayubu Damian Tewele akifanya utambulisho kwa viongozi wa Chuo kuelezea historia, tamaduni na vivutio tofauti vinavyo patikana Tanzania.

## WATANZANIA JIMBO LA TIANJIN WATUMIA LUGHA ADHIMU YA KISWAHILI KAMA UTAMBULISHO KATIKA SIKU YA UTAMADUNI

Katika maadhimisho ya siku ya utamaduni iliyofanyika Tianjin, Watanzania walipata fursa ya kutumbuiza wimbo maarufu wa “Hakuna Matata,” kama sehemu ya uwakilishi wao chuoni. Onesho hilo liliwavutia wengi na kuibua hisia za furaha.Mbali na onesho la muziki, siku hiyo ilikuwa na ushiriki wa wanafunzi wa Kichina wanaojifunza Kiswahili, wakishirikiana kwa karibu na Watanzania katika shughuli mbalimbali.

Katika banda la Tanzania, wageni walipata fursa ya kujifunza kuhusu mila, sanaa na maisha ya Kitanzania kupitia vinyago na vifaa vingine vya mikono vilivyotengenezwa kwa malighafi asilia kutoka nyumbani. Watanzania pamoja na wanafunzi wa Kichina wanaojifunza Kiswahili walishirikiana kwa pamoja kuelimisha wageni, huku wakieleza maana na historia ya kila kipande kilicho oneshwa.

Tukio hili liliimarisha utambulisho wa Tanzania nchini China, kuonesha uhusiano wa kitamaduni na ukuaji wa lugha ya Kiswahili nnje ya mipaka ya Tanzania. Kwa pamoja, waliuonesha ulimwengu kuwa Kiswahili ni lugha rafiki, yenye lafudhi iliojaa usataarabu katika kuunganisha watu wote.



Watanzania kutoka mji wa Tianjin wakitutumbuiza wimbo wa hakuna matata.

TASAFIC MAGAZINE
MAY 2025



Mwalimu Martin wa lugha ya Kiswahili kutoka chuo kikuu cha lugha za kigeni Tianjin, akifundisha upigaji wa ngoma ya asili kutoka Tanzania.



Wanafunzi wanaojifunza Kiswahili wakiwa na mwanafunzi kutoka Comoro mwenye vazi la asili, pamoja na watanzania






Banda la watanzania katika maadhimisho ya siku ya utamaduni chuo kikuu cha Tianjin

## UTAMADUNI WETU, FAHARI YETU UGHAIBUNI WATANZANIA CHANGCHUN, JIMBO JILIN

Tarehe 17 Mei, 2025, wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Jilin Normal University walijumuika kwenye shughuli maalum ya utamaduni mji wa Changchun, Jimbo la Jilin. Katika tukio hilo, wanafunzi kutoka Tanzania walitumbuiza kwa kucheza nyimbo zenye mdundo wa asili kutoka Tanzania. Miondoko na nguvu ya kisanaa ya Tanzania viliwavutia waliohudhuria, na kuwa sehemu ya kipekee ya maadhimisho hayo.

Maonesho haya ya kitamaduni yanaendelea kuwa jukwaa muhimu kwa Watanzania nchini China kuonesha urithi wao, kushiriki matukio tofauti na kujenga uhusiano mzuri na mataifa mengine, hasa kupitia sanaa ya maonesho.



Wanafunzi wa Jilin Normal University wakiwa katika picha ya pamoja



Wanafunzi wa Tanzania wakiwa jukwaani katika siku ya utamaduni chuo cha Jilin Normal University


Wanafunzi wa kigeni kutoka mataifa tofauti katika Chuo cha North East University wakiwa katika picha ya pamoja.


Wanafunnzi wa chuo cha Changchun Aviation University pamoja na viongozi wa jumuiya ya wanafunzi Jilin (TASAJI-Tanzanian Student Association In Jilin).

**VIONGOZI WA JUMUIYA YA WANAFUNZI JILIN WAPATA MUALIKO KUTOKA KWA WANAFUNZI WA CHUO CHA JESHI LA ANGA, CHANGCHUN AVIATION UNIVERSITY**

Katika kuendeleza ushirikiano wa kijamii na kitaaluma, viongozi wa Jumuiya ya Wanafunzi wa Tanzania Jimbo la Jilin walipata mualiko kutoka kwa wanafunzi wa Chuo cha jeshi la anga Changchun Aviation University.

Tukio lilihusisha utambulishi wa wanafunzi wapya wanao soma chuo cha Changchun aviation university kama sehemu ya watanzania waishio Jilin China, hata hivyo uongozi mpya ulipata nafasi ya kujitambulisha kujenga ukaribu na watanzania wote. Kupitia uhusiano wa aina hii, wanafunzi huimarika si tu kwenye elimu, bali hata maswala ya kijamii yakiwa na mlengo wa kutunza nidhamu, maadili, na mitazamo ya kitanzania.

TASAFIC MAGAZINE
MAY 2025

TASAFIC MAGAZINE
MAY 2025

**KAMATI ILIOANDAA JARIDA LA TASAFIC MAY 2025**



Heda Augustino Chale, Mwenyekiti
Msimamizi wa makala



Isack Ibrahim Mrisho, M/Mwenyekiti
Mwandishi wa makala



Martin Faustin Itangaja, Katibu
Mhariri wa makala



Zaitun Abubakari, Mjumbe
Mkaguzi wa makala




Delvina Meshili, Mjumbe
Mkaguzi wa makala



Damari Madar Jeremiah, Mjumbe
Mkaguzi wa makala



Neema Oberlin, Mjumbe
Mkaguzi wa makala



Jotham Josephat Kimondo
Mkaguzi wa makala



Gloria Michael Meiseyeki
Mkaguzi wa makala